Teacher.co.ke

## SWALI LA INSHA (ALAMA 20)

Andika kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali hii: ***Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.***

**1 .Kisa kinafaa kioane na methali**

**2. Mwanafunzi aonyesha sehemu zote mbili za methali.**

**3. Dhana ya asiyeskia la mkuu ionekane vizuri.**

**4. Dhana ya kuvunjika guu ijitokeze hata kama ni aya chache .**

**Maana : Asiyefuata ushauri huwa hana mwisho mwema.**

**Mfano wa kisa : mtoto aliyelelewa vyema akaasi ushauri wa wazazi kisha mwishowe akataabika.**

**Tanbihi:**

- **Anayeshughulikia upande mmoja wa methali asipite alama C+ 10/20**
- **Kisa kisipolenga maana batini ya methali atakuwa amepotoka kimaudhui. Atuzwe D 03/20**
- **Atakayesimulia kisa kisichomhusu binadamu (pengine mnyama fulani) atakuwa amepotoka kimaudhui. Atuzwe D 03/20**
- **Atakayekariri au kunakili swali atuzwe D 02-01/20**

Teacher.co.ke

## UFAHAMU (ALAMA 10)

1. Kichwa mwafaka – Maradhi au Magonjwa
2. Aina tatu za magonjwa – **Utapia mlo, kisunzi, ukosefu wa damu, upele kuparara na kubambuka ngozi , surua, kifaduro, kupooza miguu, malale, malaria, mafua,kuumwa na kichwa, UKIMWI, kipindupindu, kifua kikuu,tauni,ukoma, kichocho,kuhara damu na safura.**
3. Hasara za Magonjwa:
    - **Kupoteza hamu ya kula.**
    - **Kichefuchefu na kutapika.**
    - **Kusononesha.**
    - **Kokonda.**
    - **Woga kwa kufikiria kifo.**
    - **Kutengwa na wagonjwa na kutamani kufa.**
    - **Kuzorotesha maendeleo.**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

4. Njia za kushikwa na maradhi:
    - Kung'atwa na wadudu.
    - Kula chakula kichafu.
    - Ukosefu wa chakula.
5. Atakumbwa – Atapatwa

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 20)

a. Tofautisha kati ya sauti hizi:

/m/ na /th/ (alama 1)

- /m/ ni king'ong'o ilhali /th/ ni kikwamizo.
- /m/ hutamkiwa midomoni ilhali /th/ ni ya ulimi na meno.
- /m/ ni ghuna ilhali /th/ ni si ghuna.

/o/ na /u/ (alama 1) /o/ hutamkiwa nyuma kati ilhali /u/ hutamkiwa nyuma juu.

b. Tenga silabi kwenye neno hili : ***muhtasari*** (alama 1)

Muh-ta-sa-ri

c. Onyesha majukumu mawili ya kiimbo kisha utolee mifano. (alama 2)

Swali - Unaitwa nani?

Taarifa - Unaitwa nani.

Hisia - Unaitwa nani!

d. Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 3)

timothy alienda shuleni tarehe 22 10 2021 akasoma kiswahili kingereza na hesabu

Timothy alienda shuleni tarehe **22/10/2021** akasoma**:** **K**iswahili,**K**ingereza na **H**esabu**.**

e. Onyesha miundo yoyote miwili ya ngeli ya A-WA kisha utolee mifano. (alama 2)

M-WA Mtu - watu

KI-VI Kipofu vipofu

CH - VY Chura - Vyura

f. Tambua aina za maneno kwenye sentensi hii. (alama 2)

**Huyu mdogo alienda shuleni.**

Huyu - Kiwakilishi

Mdogo - kivumishi

Alienda - kitenzi



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Shuleni - kielezi

g. Onyesha viambishi awali ,mzizi na viambishi tamati kwenye neno hili: ***alipikiwa*** (alama 2)

Awali a- li

Mzizi pik

Tamati iw - a

h. Nyambua vitenzi hivi kwenye kauli zilizowekwa kwenye mabano.

Kimbia (tendesha) (alama 1) kimbiza

tembea (tendeana) (alama 1) tembeleana

i. Eleza maana ya sentensi. (alama 1) Sentensi ni utungo wenye kiima na kiarifa.

**j.** Taja aina zozote mbili za sentensi. (alama 1)

- Sentensi sahili
- Sentensi ambatano
- Sentensi changamano

k. Tambua Kundi Nomino na Kundi tenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mwanafunzi huyu mfupi atapewa zawadi kesho.

**Mwanafunzi huyu mfupi – Kundi nomino**

**Atapewa zawadi kesho – kundi tenzi**

## FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)

i. Eleza maana ya fasihi. (alama 1) Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu.

ii. Taja tanzu mbili kuu za fasihi. (alama 1)

- Fasihi Simulizi
- Fasihi andishi

iii. Andika tofauti zozote tano za tanzu ulizotaja hapo juu. (alama 5)

a) Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo ilhali fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
b) Fasihi simulizi huhifadhiwa akilini ilhali fasihi aandishi huhifadhiwa kwa maandishi.
c) Fasihi simulizi ni mali ya jamii ilhali fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi/mwandishi.
d) Fasihi simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti ilhali fasihi andishi ina wahusika binadamu kwa kiasi kikubwa.
e) Fasihi simulizi ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

f) **Uwasilishaji wa fasihi simulizi huweza kuandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo n.k ilhali ule wa fasihi andishi hauandamani na utendaji isipokuwa inapowasilishwa mbele ya hadhira.**
g) **Fasihi simulizi huwasilishwa mbele ya hadhira ilhali fasihi andishi si lazima iwasilishwe mbele ya hadhira.**
h) **Fasihi simulizi huwasilishwa mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini, n.k ilhali fasihi andishi haina mahali maalum.**
i) **Fasihi simulizi huandamana na shughuli fulani ya kitamaduni ilhali fasihi andishi haiandamani na shughuli ya kitamaduni.**
j) **Fasihi andishi huhitaji muda kutunga ilhali baadhi ya fasihi simulizi huzuka papo hapo k.m. semi, maigambo.**
k) **Fasihi simulizi ina uwezo mkubwa wa kubadilishwa na fanani anapowasilisha ufaraguzi) bali fasihi andishi haibadiliki isipokuwa mwandishi aiandike upya.**
l) **Fasihi simulizi ina historia ndefu kuliko fasihi andishi kwa kuwepo tangu mwanzo wa maisha ya binadamu.**
m) **Fasihi simulizi huwasilishwa wakati maalum k.v. usiku, kipindi fulani cha mwaka ilhali andishi haina wakati maalum.**

iv. Taja umuhimu wa fasihi kwa jamii. (alama 3)

a) **Kuburudisha-kustarehesha, kufurahisha, kuchangamsha, kutuliza, kusisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili - nyimbo, hadithi, vitendawili**
b) **Kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.**
c) **Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.**
d) **Kufariji k.m mbolezi na methali k.m. 'Baada ya dhiki faraja'.**
e) **Vipengele vya fasihi simulizi k.v mashairi, nyimbo, nahau, hutumiwa katika uandishi wa fasihi andishi.**
f) **Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k.**
g) **Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v soga, methali, n.k.**
h) **Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili 'Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.' - Mtu hawezi kumwoa dadake.**
i) **Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.**
j) **Kukuza lugha k.v. misimu inapokita kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.**
k) **Kukuza uwezo wa kutumia lugha kadiri mtu anapoendelea kuwasilisha k.v. hotuba, vitanza ndimi husaidia kuboresha matamshi na kutofautisha maana za maneno.**
l) **Kuza uwezo wa kubuni k.v. malumano ya utani, vitanza, ndimi ngonjera, n.k.**
m) **Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.**
n) **Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.k.**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

## ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

isimujamii (alama 1)

**Taaluma inayochunguza uhusiano kati ya jamii na lugha.**

sajili ( alama 1)

**Matumizi ya lugha katika muktadha Fulani.**

b) Taja kaida zozote tatu za lugha (alama 3)

- **Jinsia/uana**
- **Umri**
- **mazingira**

c) Orodhesha sifa zozote tano zinazotumiwa katika lugha ya shule. (alama 5)

- **Lugha ya heshima.**
- **Mazungumzo hutokea kwa zamu.**
- **Msamiati maalum.**
- **Matumizi ya sentensi ndefu.**
- **Lugha ya kuamuru.**

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes